# Kisiwa cha Mafia kuwa kitovu cha uchumi wa bluu – Majaliwa




*MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge (mwenye t-shirt nyeupe) akimkabidhi Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, zawadi ya sanamu ya samaki aina papa potwe wakati alipofika kufunga maonyesho ya Wiki ya Utalii, Biashara na Uwekezaji katika Uchumi wa bluu katika fukwe za bahari ya Hindi huko Kijiji cha Utende, wilayani Mafia mkoani Pwani (Picha na Scolastica Msewa).*

Kisiwa hiki kimebarikiwa na kina fursa nyingi zinazotokana na mali za mazao ya bahari ambayo umekuwa ndio ufunguo kwenye ujenzi wa uchumi wa bluu.

**NA SCOLASTICA MSEWA**

WAZIRI Mkuu Kassimu Majaliwa amesema Kisiwa cha Mafia ni kitovu cha uchumi wa bluu kutokana na uwepo wa mazao mengi ya bahari katika kisiwa hicho.

Majaliwa ameyasema hayo wakati akifunga kongamano la Wadau wa Uwekezaji katika Utalii na Uchumi wa Bluu katika Kisiwa cha Mafia lililo ambatana na maonyesho ya siku tatu za shughuli mbalimbali za wadau wa uwekezaji wa utalii nchini.

Amesema vivutio vilivyopo wilayani Mafia ni vivutio vya uchumi wa bluu na uwepo wa fursa nyingi za bahari.

"Kisiwa hiki kimebarikiwa na kina fursa nyingi zinazotokana na mali za mazao ya bahari ambayo umekuwa ndio ufunguo kwenye ujenzi wa uchumi wa bluu.

"Mnatumia vizuri fukwe kwa kukaribisha utalii katika uwekezaji, kwa upande mwingine kauli hii ni wito kwa wananchi wa Wilaya Mafia kuchangamkia fursa zinazotokana na mazao ya bahari ili waweze kuimarika kiuchumi.

Ameongeza kuwa: "Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa akihamasisha uchumi wa mtu mmoja mmoja wa kikundi lakini na wilaya kwa ujumla ili kufikia mafanikio."

"Ili tuweze kuwa na uchumi mzuri ni lazima kila mmoja ashiriki katika uwekezaji kwenye uchumi wa bluu yaani utalii, uvuvi au namna nyingine katika kujipatia kipato," anasema.

Amesema lengo la wiki ya uchumi wa bluu kwa Mafia ni kuhamasisha utalii kwenye fukwe, visiwani na malikale zilizopo baharini kama vile matumbawe hai na papa potwe.

"Lazima tumtangaze (Papa potwe) mmefanya vizuri nilipofika pale mjini nikakuta sanamu na picha mmeweka kuonyesha kwamba ukimuona samaki yule ujue Mafia ni burudani," amesema Majaliwa.

Amesema maonyesho hayo ni miongoni mwa fursa muhimu kwa Wana Mafia na mkoa wa Pwani kwa ujumla wake.

Amebainisha kuwa kwa mujibu wa takwimu, Mafia inaongoza kwa samaki wengi na viumbe mbalimbali vya baharini ambavyo adimu.

"Kwa mantiki hiyo kisiwa hiki kinachangia pato kubwa kwenye uchimu wetu wa bluu na mnaongezea pato la taifa. Nataka niwasihi msiache shughuli za uvuvi maana zinatuletea uchumi," anaeleza.

Kwa upande wa utalii, anasema takwimu zinaonyesha kuwa kuna ongezeko kubwa la watalii wanaotembelea Mafia kwa sasa kwani tangu mwaka 2020 mpaka sasa, watalii 14,155 wamefika ikiwa ni niongezeko kubwa.

Waziri Mkuu amesema kuwa watalii hao wameingiza pato la sh. bilioni 2.7 ambao wengi wamefika kisiwani hapo ikiwa ni sehemu ya matunda ya filamu ya Rayol tour.

"Nitoe wito kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani na Kisiwa cha Mafia tangazeni fursa zenu, onyesheni mliyonayo kupitia mifumo ya matangazo ili watalii wengi zaidi waweze kuja na serikali itawaunga mkono," amebainisha.

Majaliwa amemuagiza Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, serikali ivirejeshe visiwa na viwanja kisiwani hapo ambavyo vimeng'ang'aniwa na wawekezaji miaka mingi bila kuendelezwa kwa kutofanyika chochote ili vigawiwe kwa wawekezaji wengine.

Amesema hatua hizo zifanyike kwa kuzingatia taratibu na sheria za nchi kwani muda wa mwekezaji kumiliki eneo la uwekezaji bila kuendeleza ni miezi 36.

"Kweli nyinyi mnawaacha tu? sheria si zipo? watu wa ardhi si mpo?," Mkuu wa mkoa uwekezaji katika viwanja ni miezi 36 hujaendeleza nyang'anya chukua tunampa mtu mwingine.

Ameongeza kuwa: "Wakuu wa wilaya mwende mkaainishe maeneo ya fursa za uwekezaji wa utalii mliyonayo yaliyoshikiriwa na wawekezaji kwa miaka mingi bila kuendelezwa kwani sisi tunatangaza fursa za uwekezaji wa utalii lakini wengine wanaturudisha nyumba."

## UIMARISHAJI USAFIRI WA ANGA NA MAJINI

Waziri Mkuu amesema serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri wa anga na baharini katika Kisiwa cha Mafia ambapo imetenga sh. bilioni 9.5 ya kutengeneza kivuko kipya chenye uwezo wa kubeba mizigo ya tani 120 pamoja na abiria 500 kwa wakati mmoja.

Ameeleza kwa sasa mchakato wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi unaendelea ili kazi ianze mara moja na utengenezaji wa kivuko hicho kikamilike kwa wakati.

"Katika kuinua uchumi wa Mafia, serikali inaboresha Uwanja wa Ndege wa Mafia kwa kuongeza taa ili usafiri kuwa wa uhakika wakati wowote na kuongeza jengo la abiria liweze kufikia kuhudimia watu 200 kwa wakati mmoja," amesema.

Akizungumzia sekta ya kilimo amehimiza kilimo cha mwani, korosho huku akiwaasa wananchi kisiwani humo kujikita katika kilimo hicho na shughuli za uvuvi ambavyo vina tija katika masoko.

Pia, ameshauri tamasha hilo lisiishie hewani liwe endelevu kwa kila Septemba ya kila mwaka ili kuendelea kutangaza fursa zilizopo wilayani humo.

Awali, akimkaribisha Waziri Mkuu, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, ameeleza dhumuni la kuwepo kwa tamasha hilo.

"Hili tunalofanya ni kutafsiri kwa vitendo azma ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kufungua Wilaya ya Mafia katika uwekezaji wa uchumi wa bluu na utalii. Imani yetu mwaka mmoja matokeo chanya yataonekana," amesema Kunenge.

Mbunge wa Jimbo la Mafia (CCM) Omary Kipanga, amemshukuru Rais Dk. Samia kwa fedha zilizoletwa wilayani Mafia katika kipindi cha miaka miwili na miezi nane ambapo zaidi ya sh. bilioni 45 zimefika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

CS CamScanner